

# SOMO LA 1

KITABU CHA MWEZESHAJI

KOZI YA "JUKUMU LA KUJIZIDISHA"

Kupanda Makanisa Yenye Afya

MAELEKEZO YA KUZINGATIA: Kitabu cha Mshiriki kina nafasi zilizo wazi kwa ajili ya kila neno lililopigiwa mstari katika kitabu cha mwezeshaji. Majibu yameorodheshwa chini ya ukurasa wa kitabu cha somo. (Maelekezo haya hayapo kwenye toleo la pdf la kitabu hiki).



**Mtando wa Kuzidisha**  
*Makanisa Mengi Zaidi, Makanisa Yenye Nguvu*

**"JUKUMU LA KUZIDISHA"**

MAELEZO YA MTAALA WA KUPANDA KANISA | OMEGA – M/N/M

SOMO LA 1 PANDA KANISA LENYE AFYA	KUANDAA KUSHIRIKISHA HABARI NIEMA	MUNGU	KUWAELEKEZA WATU KUELEKEZA KWENYE IMANI	SOMO LA 5 KUWAELEKEZA WATU KUELEKEZA KWENYE IMANI
IBADA	Misingi ya Kibilia ya Makanisa Yenye Afya	Misingi ya Kitheolojia ya Makanisa Yenye Afya	Misingi ya Kimkakati ya Makanisa Yenye Afya	Misingi ya Kimkakati ya Makanisa Yenye Afya
SEHEMU YA 1	KANSA LENYE AFYA NI NINI?	RAMANI YA KIROHO: KANUNI ZA UTAFITI WAKO	HAKI KWA IMANI	VIZUZI VYA INJILI
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi/Usahihhi	Kazi, Andiko, na Muktadha	Tambuliwa Katika Wito wa Kimungu	Uninjili, Uanafunzi
SEHEMU YA 2	NANI MPANDA KANISA LENYE AFYA	HIKI NDICHO YESU ALICHONIFANYA! KUELEZE NA KUSHIRIKISHA USUHUDA USUHUDA WAKO BINAFSI	MUNGU ANANIONYESHA NINI? SHIRIKISHA USUHUDA WAKO NA MTEMBEYO WAKO WA MAOMBII	MCHAKAKATO WA KUBADILKA I
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Tambuliwa Katika Wito wa Kimungu	Uninjili	Kazi, Andiko, na Muktadha	KUWALIMARISHA / kuwawezesha viongozi
SEHEMU YA 3	KUFIRIKI – Z: MUNGU ANATAKA NINI?	KUONGGOZA VIKUNDI VIDOGO	MPANGO WANGU MIKUU WA KUPANDA KANISA: KUTAMBUA MAONO YA MUNGU	UNINJILI NA KUPANDA KANISA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihhi	Uninjili, Uanafunzi, Kuwawezesha / Kuwalmarisha viongozi	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihhi	UNINJILI
SEHEMU YA 4	MZUNGUKO WA KUPANDA KANISA	NJIA YA II YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: KUANGALIA NENO LA MUNGU	MPANGO WANGU MIKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA KAZI	KUANZISHA KIKUNDI KIDOGO
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihhi	Uninjili, Uanafunzi	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihhi	UNINJILI NA KUFIKIA MAHTAJI YA JAMII
SEHEMU YA 5	KWA NINI VIKUNDI VIDOGO?	NAMNA YA KUTENGENEZA MAOMBII KATIKA UPANDAJI WAKO WA KANISA	MPANGO WANGU MIKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA MSINGI	UZOEFU WA KIKUNDI KIDOGO
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Uninjili, Uanafunzi	Uninjili	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihhi	UNINJILI
SEHEMU YA 6	NJIA YA I YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: HEBU BIBLIA ITUFUNDISHE	TAMASHA LA MAOMBI: ZABURI 95	MPANGO WANGU MIKUU WA KUPANDA KANISA: MAANA YA MKAKATI	NJIA YA III YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA ELEKEZI: KUTAFSIRI NENO LA MUNGU
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Uninjili, Uanafunzi	Kuabudu	Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahihhi	Uninjili, Uanafunzi

	SOMO LA 7 TENGENEZA TIMU	SOMO LA 8 TENGENEZA TIMU	SOMO LA 9 KUWAJALI WATU	SOMO LA 10 KUANZISHA KANSIA	SOMO LA 11 KUPANGA KWA AJILI YA MAMBO YAJAYO	SOMO LA 12 KUENDELEA MBELE KWA UMOJA
BADA	Kubadilishwa na Injili	Neema ni kwa wanyenyekevu	Upendo, Msingi wa Huduma	Ili Ulimwengu Upate Kuamini: Yohana 17	Kuhesabu Gharama	Mpaka Ulimwengu Wote Usikie!
SEHEMU YA 1	MISINGI YA KIBIBIA YA KANISA	KAZI YA TIMU: KUFANYA KAZI NA WENGINE KWA USAHIHI	UINJILISTI WA KIMAHUSIANO	KAZI ZA USHIRIKA ZA KANISA	UTANGUIZI KATIKA UWAKILI	KUTATUA MAZINGIRA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganylko wa Mawazo	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwajali washirika wa kikundi kidogo	Mchanganylko wa Mawazo	Uwakili wa Rasilimali	Ushirika
SEHEMU YA 2	KIUMBIE HAI	KUANZISHA TIMU	USHIRIKA	HUDUMA KUPITIA KARAMA ZA KIROHO	UWAKILI WA FEDHA	TOBA KAMA NAMNA YA MAISHA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganylko wa Mawazo	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Ushirika	Kuanganisha Mwili Kutokana na Karama za Kiroho	Uwakili wa Rasilimali	Ushirika
SEHEMU YA 3	KIKUNDI CHA WATU KINAKUWA KANISA LINI?	UHAI KATIKA MIADALA WA KIKUNDI KIDOGO	KUJUJU JAMII YETU	NAMNA YA KUTUMIA TATHMINI YA KARAMA ZA KIROHO		TOBA NA UREJESHO: NIDHAMU YA KANISA
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Mchanganylko wa Mawazo	Uanafunzi	Uinjilisti, Andiko, na Muktadha	Kuanganisha Mwili kutokana na Karama za Kiroho		Ushirika
SEHEMU YA 4	NJIA YA V YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NUJA ELEKEZI: NJIA ZA KUTUMIA MAFUNZO ELEKEZI YA KUJIFUNZA BIBLIA	KUWAFUNDISHA VIONGOZI WAPYA WA VIKUNDI VIDOGO	TABIA ZA KANISA LINALOKUWA	UHAI WA VITA VVA KIROHO		MITINDO YA UONGOZI
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Uanafunzi	Uanafunzi, Kuimarisha/ Kuwawezesha Viongozi	Mchanganylko wa Mawazo		SEMINA YA MPANGO MIKAKATI	Kuwawezesha / Kuwaimarisha Viongozi
SEHEMU YA 5	MWONEKANO WA KIONGOZI MKRISTO	MITINDO YA KUJICHANGANYA	UONGOZI WA KITUMISHI	NAMNA YA KULIONGOZA KANISA KATIKA KUABUDU		KANISA LETU NA UKUBWA WA MWILI WA KRISTO
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuwawezesha / Kuwaimarisha viongozi	Kuabudu		Ushirika
SEHEMU YA 6	MAHUBIRI YA KIBIBIA I: KUELEVWA UIJUMBE	MAHUBIRI YA KIBIBIA II: KULELEWA KUNDI / KUSANYIKO	TAMASHA LA MAOMBI: WAEEFESO 3 – 5	MAHUBIRI YA KIBIBIA III: KUIJIELEWA WEWE MWENYEWYE		TAMASHA LA MAOMBI: KUOMBIA KUENEZA INILI
WAZO LA KANISA LENYE AFYA	Kuabudu	Kuabudu	Ushirika	Kuabudu	Uwakili wa Rasilimali; Kuzungumzia Maono kwa Uwazi / Usahizi	Unjilisti

**JUKUMU LA KUJIZIDISHA**  
**Masomo ya Kupanda Makanisa Yenye Afya**  
**Huduma ya Mtando wa Kujizidisha**  
**Makanisa Mengi Zaidi/Makanisa Yenye Nguvu Zaidi**  
Hatimiliki© 2015



Mafunzo haya ya mpanda Kanisa ni mchanganyiko wa Kozi ya Omega Iliyofupishwa na Somo la Kupanda Makanisa Yenye Afya ya Mtando wa Kuzidisha.

MNM imepata kibali kutoka kwa Kituo cha Mafunzo Kwa Wapanda Kanisa (TCCP) na kutoka Huduma kwa Ulimwengu (World Ministries) kuandaa kazi hii kwa matumizi ya Kanisa.

Unaruhusiwa **na unatiwa moyo kuzalisha na kugawa somo hili katika mtindo wowote** uliotolewa kwa namna ambayo: (1) utajali chanzo, (2) utaonyesha ikiwa mabadiliko yamefanyika, (3) hautatoza gharama inayopita kiwango cha uzalishaji, na (4) hautazalisha nakala zaidi ya 1,000.

OMEGA Course:  
Practical Church Planter Training

Copyright © 2000, 2006 United World Mission.

Masomo haya yalinakiliwa kwanza na The Alliance for Saturation Church Planting na yakaandaliwa na ubia huo kwa ushirikiano na Peter Deyneka Russian Ministries, Project 250.

Ikiwa ungependa kuyaweka masomo haya kwenye mtando ama ikiwa matumizi yako lengwa ni tofauti na yaliyotajwa hapo juu, tafadhalu wasiliana na United World Mission, ATTN: Jay Weaver/Omega, 9401-B Southern Pine Blvd., Charlotte, NC 28273-5596, au omega\_course@alliancescp.org.

Kutafsiri na kuasili kulingana na muktadha wako vinatiwa moyo pia.

Tunamshukuru Dr. Jerry Wofford na Dr. Jeff Hale kwa mchango mkubwa kwa maandalizi ya kazi hii.

Gary Teja na Juan Wagenveld, Wahariri wa Jukumu la Kuzidisha.

[www.multiplicationnetwork.org](http://www.multiplicationnetwork.org)

<b>PENDEKEZO LA MUUNDO WA SIKU 1 WA MAFUNZO YA SOMO LA 1</b>		
	UTANGULIZI WA SOMO LA 1	2:00
	IBADA	2:15
	KUTOA TAARIFA	2:30
KIPINDI CHA KWANZA	KANISA LENYE AFYA NI NINI?	3:00
	MAPUMZIKO	4:00
KIPINDI CHA PILI	MPANDA KANISA MWENYE AFYA YUKOJE?	4:15
KIPINDI CHA TATU	WAZO LA "Z": MUNGU ANATAKA NINI?	5:15
	CHAKULA CHA MCHANNA	6:15
KIPINDI CHA NNE	MZUNGUKO WA UPANDAJI WA KANISA	7:15
KIPINDI CHA TANO	KWA NINI VIKUNDI VIDOGO?	8:15
	MAPUMZIKO	9:15
KIPINDI CHA SITA	KUACHA BIBLIA ITUFUNDISHE: MBINU YA KUJIFUNZA BIBLIA KWA NJIA YA UCHIMBUZI, SEHEMU YA 1	9:30
	KUFUNGA	10:30
	MWISHO WA SIKU	10:45

## UPANDAJI WA KANISA LENYE AFYA

### Somo la 1

**Makusudi ya Mafunzo:** Washiriki wataweza kueleza kwa maneno yao,

- Kanisa lenye afya ni nini ;
- Kwa nini ni muhimu kupanda kanisa lenye afya; na
- Hatua za msingi katika kupanda kanisa lenye afya

### Utangulizi wa Somo la 1 (Dakika 15.)

Maoni ya Utangulizi ya Mwezeshaji (Dakika 2.)

- Wakaribishe washiriki kwa namna ya ucheshi, urafiki na kwa uchangamfu.
- Waongoze washiriki katika maombi mafupi ya pamoja, mkiweka wakfu siku hiyo kwa utukufu wa Mungu.

### Kuijua Shughuli yako (Dakika 5 .): Maneno matatu

- Waombe washiriki kuchagua maneno matatu yanayowaelezea wao wenyewe.
- Waambie washiriki ni watu wangapi wamo kwenye kikundi na kwamba wana dakika 4 za kushikana mikono kwenye chumba, kujitambulisha na kushirikisha maneno yao matatu.
- Mwishoni, angalia ni watu wangapi hasa waliofanikiwa kushirikishana katika chumba. Unaweza kuuliza idadi ya watu walioshirikishana nao. Kwa mfano, ikiwa kuna washiriki 20, Ni wangapi walioshirikisha watu 10 au zaidi, watu 15, watu 20? Sherehekeeni na kuufurahia wakati huu.

### Mfano :

Habari , jina langu ni Mariamu.

Naweza kujielezea mwenyewe kuwa ni mbunifu, mkarimu na mchapa kazi

## **Shughuli ya Makanisa Yenye afya na Yasiyo na Afya (Dk 8.)**

Muhimu Kwa Mwezeshaji: Kusudi la shughuli hii ni kuwasaidia washiriki kuanzisha mwelekeo wa haraka unaolenga juu ya maarifa, ujuzi, na mitazamo inayotakiwa kwa ajili ya kupanda Kanisa lenye afya.

- Sema, "Kila mmoja wenu analeta utajiri wa uzoefu wa makanisa kwenye kozi ya wapanda kanisa wenu. Shabaha ya funzo hili ni kukusaidia kuelezea sifa za Kanisa lenye afya na vitu vinyayohitajika ili kupanda kanisa lenye afya."
- Ligawe kundi kubwa katika vikundi 2 vidogo. Ndani ya dakika 4, waombe kikundi A waorodheshe sifa nyingi kadiri wawezavyo za Kanisa lenye afya wanazoweza kuzikumbuka kulingana na uzoefu wao. Vilevile, waombe kikundi B kuorodhesha sifa ama tabia nyingi iwezekanavyo za Kanisa lisilo na afya wanazoweza kuzikumbuka kulingana na uzoefu wao.
- Ruhusu dakika moja kwa kila kikundi kutoa orodha ya sifa zao.
- Mwambie kila mmoja, "Leo tutakuwa tukijifunza juu ya sifa 10 ambazo Mtandao wa Kuzidisha (Multiplication Network) iliona ni sifa au tabia za msingi za Kanisa lenye afya. Hata hivyo, kwanza tutatafakari kwa pamoja sababu tano za msingi za Kibiblia za kupanda Kanisa lenye afya."

## KUFANYA IBADA

### Misingi ya Kibiblia Kwa Makanisa Yenye Afya (Dk.15 )

**Maelekezo ya Mwezeshaji:** Toa vifungu nya Biblia kwa kila sababu ya kibiblia kwa washiriki mbalimbali. Waombe wasome vifungu nya Biblia kwa sauti. Waongoze wana kikundi kugundua kila sababu ya kibiblia kutoka kwenye vifungu viliviyosomwa na wajaze kwenye nafasi za majibu zilizo wazi kwenye vitabu vyao.

### Shughuli ya Ufunguzi (Dk. 2 )

Waombe washiriki washirikishe mawazo yao juu ya sababu za kupanda makanisa mapya. Waombe kusikiliza ili waone ni sababu zipi kati ya hizo zimetajwa katika kipindi hiki.

### Ibada ya Kujifunza Biblia ( Dk. 13 )

Kuna sababu tano za Kibiblia za kupanda makanisa mapya na yenye afya:

#### 1. Kwa sababu Mungu ni Baba ambaye huwatafuta na kuwapata waliopotea.

Mistari ya Msingi | Mwanzo 3:9; Zaburi 23; Luka 14:15-24

#### 2. Kwa sababu upendo wa Kristo hutubidiisha.

Mistari ya Msingi | 2 Wakorintho 5:14-20; Mathayo 18:12-14; Yohana 14:23

#### 3. Kwa sababu Roho Mtakatifu ametumwa kwa watu wote.

Mistari ya Msingi | Matendo 2:5-11; 10:44-48; 1:8

#### 4. Kwa sababu kanisa la mahali ni tawi la Ufalme wa Mungu.

Mistari ya Msingi | 1 Petro 2:5, 9-10, 12; Wakolosai 1:13-23;  
Warumi 12:4-8

#### 5. Kwa sababu kupanda makanisa mapya kunampa Mungu utukufu.

Mistari ya Msingi | Waefeso 1:1-14; Ufunuo 7:9-12

Maelekezo ya Jumla ya Mwezeshaji: Kwa sababu hakuna ripoti inayotakiwa katika funzo hili, tumia muda 1) kutoa wazo la jumla la kozi hii na 2) kuelezea umuhimu wa ripoti na fomu zitakazotumika kwa mafunzo yote .

BABA - HUWATAFUTA - KUWAPATA - KRISTO - ROHO MTAKATIFU - TAWI - UFALME  
- MUNGU - UTUKUFU

Kulitumia Wazo Kuu la Kupanda Makanisa Yenye Afya katika Kozi ya Jukumu la Kuzidisha (Dk. 15)

---

---

---

---

**Maelekezo:**

- Waombe washiriki kurekodi Hatua Tano zifuatazo za Kupanda Kanisa katika mchoro uliotolewa kitabuni. Anza na hatua ya kwanza, uinjilisti, na uendelee hadi hatua ya mwisho, kuabudu na huduma.

### **Hatua Tano za Upandaji wa Kanisa**



**Maelekezo:**

- Waongoze washiriki kwenye Muhtasari wa Kozi mwanzoni mwa kitabu cha somo.
- Elezea muundo wa kozi ( mafunzo 12 yenye vipindi 6 kwa kila funzo).
- Waombe washiriki kusoma vichwa vya habari vya vipindi 6 vya kozi au funzo la 1. Waulize ni jinsi gani wangeweza kuhusianisha kila kipindi na Hatua Tano za Upandaji wa Kanisa.
- Pitia tarehe na mambo mengine muhimu yanayohusiana na kukamilisha mafunzo 12.
- Pata muda wa kujibu maswali kutoka kwa washiriki kwa habari ya mtindo na maudhui ya kozi na mambo mengine muhimu.

*Muhtasari wa Ripoti ya Kupanda Makanisa Yenye Afya (Dk. 15 )*

## **KUTOA RIPOTI: (Dk. 30 )**

### **Maelekezo:**

- Warejeshe washiriki kwenye ukurasa katika kitabu chao cha somo chenye ABC za Mpanda Kanisa : Ripoti ya Kila Mwezi. Elezea umuhimu wa utoaji wa ripoti kwa ajili ya kozi.
- Elezea namna ya kujaza fomu.
- Elezea namna wana kikundi watakavyopeana ripoti wakati wa Kipindi cha Kutoa taarifa kwenye funzo la 2 hadi la 12.

## ABC ZA MPANDA KANISA

### TAARIFA YA MWEZI

### TAARIFA ZA KAWAIDA

MWEZI WA TAARIFA		USIMAMIZI WA MAHUDHURIO YA VIKAO	NDIYO	HAPANA
JINA LA MPANDAJI				
KANDA YA MPANDAJI				
MRATIBU WA KANDA				

### BINAFSI

<b>WATU WAPYA WALIOFIKIWA</b> WATU WALIOFIKIWA KWENYE MAZINGIRA YA KUPANDA MAKANISA KULETA INJILI	
<b>WAONGOFU WAPYA</b> WAFUASI WA YESU	
<b>WATU WAPYA WALIOBATIZWA</b> WATU WALIOSHIRIKI KWENYE SAKRAMENTI YA UBATIZO	
<b>VIONGOZI WAPYA KATIKA MAFUNZO</b> WATU WANAOFUNDISHWA UONGOZI NA WAPANDAJI	

### VIKUNDI VIDOGO | Kiwango cha chini wafuasi 2 wapya na kiongozi mmoja

<b>VIKUNDI VIDOGO VIPYA</b> VIKUNDI VILIVYOANZISHWA MWEZI HUU	
<b>WASHIRIKI WAPYA KATIKA VIKUNDI VIDOGO</b> WATU WAPYA WALIOSHIRIKI KATIKA VIKUNDI VIDOGO MWEZI HUU	
<b>VIONGOZI WAPYA NA KIKUNDI</b> VIONGOZI WAPYA NA KIKUNDI CHINI YA USIMAMIZI WA MPANDAJI	

### MAOMBI UNAYOHITAJI

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_

### SHUHUDA

---



---



---



---



---



---

# KIPINDI CHA 1

## KANISA LENYE AFYA NI NINI? (DK. 60)

### MFANO WA SOMO: SIMULIZI YA KANISA LISILO NA AFYA (DK.10 )

Zingatio kwa Mwezeshaji: Mfano wa Somo huwaongoza washiriki kuhisi hali halisi ya matatizo ya maisha ili kwamba washiriki waongeze uelewa wa sifa 10 za Kanisa lenye afya. Mfano wa Somo huanza kwa kuelezea Kanisa lisilo na afya, hasa Kanisa lilopandwa kwa njia zisizo na afya.

Maelekezo:

- Waombe washiriki kusoma “Simulizi ya Kanisa Lisilo na Afya.”
- Waombe washiriki kuelezea baadhi ya viashiria vya hali ya Kanisa lisilo na afya .
- Jadili pamoja na washiriki namna viashiria hivi vinavyohusiana na Hatua 5 za Upandaji wa Kanisa.
- Waulize, “Ni lini Kanisa hili lilianza kutokuwa na afya?” Washiriki ni muhimu watambue kwamba Kanisa lilikuwa katika njia ya kutokuwa na afya tangu lilipopandwa.
- Sema, “Kusudi la kipindi hiki ni ili uweze kuongeza ufahamu wa Sifa 10 za Kanisa Lenye Afya ili kwamba uweze kuzijenga katika Kanisa lako jipya pale unapolianzisha. Tofauti na Kanisa la Hosanna (Hosanna Church), Kanisa lako litaanza na mwanzo wenye afya!”

#### *Simulizi ya Kanisa Lisilo na Afya*

Kanisa la Hossana lilipoanzishwa kwa mara ya kwanza, lilianza na migogoro na maumivu. Kulingana na historia ya Kanisa, uamuzi wa kupanda Kanisa la Hossana ultokana na migogoro kati ya kikundi kimoja cha watu waliomheshimu Mchungaji kiongozi aliystaa fu na kikundi kingine waliokuwa watiifu kwa Mchungaji kiongozi aliyepo sasa. Hatimaye, dhehebu liliamua kuligawa kusanyiko kuwa makanisa mawili. Moja ya makusanyiko mapya, baada ya muda, wakaamua kuliita Kanisa lao, Kanisa la Hossana. Mchungaji Lee akachaguliwa kuwa Mchungaji kiongozi wa kwanza wa moja ya makusanyiko mapya. Mara akakabiliana na migogoro kwa wazee wa Kanisa ambao mwishowe walihama Kanisa wakiwa na baadhi ya washirika.

Katika Kanisa hili, kila mzee alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 55. Wote, watu wazima na vijana hawakuwa na imani kabisa na uongozi wa Kanisa .

Kutokuaminiana huku ilikuwa ndio sababu mojawapo ya Kanisa la Hossana kujitenga na kusanyiko la kwanza. Kanisa la Hossana halikuyapokea mabadiliko kirahisi katika mwelekeo wa uamsho. Kadiri washirika wa Kanisa waliokuwamo walivyoendelea kuzeeka, ndivyo Kanisa la Hossana lilivyokutana na ugumu zaidi katika kufanya mabadiliko muhimu ili liwe kusanyiko lenye uhai.

Mtindo wa asili wa kuabudu ulikuwa tatizo kubwa, kwa sababu washirika wazee peke yao ndio walioufurahia. Jengo la ibada lilikuwa na uwezo wa kubeba washiriki 1000, lakini ibada ya Jumapili ilikuwa na wastani wa washirika 200 tu. Matatizo haya yalikuwa ni ishara ya kupoa.

Hali ya Kanisa kiuchumi ilikuwa mbaya. Wakati wa baridi hawakutumia kifaa cha kuongeza joto kwa sababu ya hali mbaya ya Kanisa kifedha. Wakati wa joto kulikuwa na tatizo lilelile kwa habari ya viyoyozi. Kanisa liliingia katika madeni. Mbaya zaidi, uongozi wa Kanisa haukujitolea kutoa zaka. Mfumo wa ufuatiliaji wa waongofu wapya haukuwepo tena. Vikundi vidogo vikawa ni vile tu vilivyo rasmi kwa wanawake na vikundi vingine vidogo vya washirika wa Kanisa. Vikundi hivi vilikuwa havizalishwi kupitia uinjilisti. Matatizo yanayoendelea, migawanyiko, na kutokuwa waaminifu kila mtu na mwenzake ilikuwa ndio hali ya Kanisa la Hossana. Hii inajumuisha hali ya huzuni ya Kanisa la Hossana kabla halijaingia katika mchakato wa uamsho ili kurejesha afya yake.

Imechukuliwa kutoka: Park, H. W. (2009). An effective strategy for church revitalization through a case study of Hosanna Church. (Doctoral dissertation, Liberty Baptist Theological Seminary)<sup>1</sup>.


---

<sup>1</sup> Retrieved from <http://digitalcommons.liberty.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1170&context=doctoral>

## SIFA 10 ZA KANISA LENYE AFYA (DK 40.)

Maelekezo :

- Waongoze washiriki kujaza katika mchoro ufuatao mnapojadili kila mada.
- Pia, waombe washiriki kuandika mambo muhimu katika vitabu vyao.



**Sema**, "Sifa 10 zimebeba alama tano na kazi tano." Waombe washiriki kujaza alama tano na kazi tano katika sehemu zilizotolewa katika mchoro.

**Sema**, "Hebu tuenze na alama tano" Waombe washiriki kujaza katika mchoro na kuandika mambo katika nafasi zilizotolewa wakati unaposhirikisha habari hii kwa mtindo wa hotuba.

### 1.- MAONO YALIYO WAZI

Tafsiri: Kuwa na maono ina maana kuziangalia siku za usoni na kuona picha iliyo wazi katika ufahamu juu ya kile ambacho Mungu anataka kukifanya kupitia kwako ili kufanikisha makusudi. Yake ya ukombozi.

"Kanisa huona kwa uwazi kile ambacho Mungu anataka liwe na lifanye, ili kwamba Mwili wa Kristo utumike kuakisi uumbaji wake mpya katika jamii."

Je, Mungu anataka Kanisa unalopanda liweje na lifanye nini? Wakati wa mafunzo yenu, mtaandika kauli ya dira inayotoa muhtasari kile ambacho Mungu anakuita uwe na ufanye kama Kanisa. Itumie kauli hii ili udumu katika mwelekeo wa huduma yako.

ALAMA TANO - MAONO - UONGOZI - MWILI ULIOHAMASISHWA - RASLIMALI - ANDIKO NA MUKTADHA - KANISA - KAZI TANO - UINJILISTI - UANAFUNZI - HUDUMA - USHIRIKA - IBADA - MAONO - KUONA - MUNGU - KUPITIA - MAKUSUDI - UKOMBOZI - MUNGU

## 2.- KUIMARISHA UONGOZI

Tafsiri: Uongozi wa Kikristo unaweza kueleza ifuatavyo: "Viongozi wa Kikristo ni watu waliojitoa kwa **Mungu** (tabia), wanaojua ni **wapi** wanakokwenda (dira), na wenye **wafuasi** (ushawishi)."

"Kanisa hutumikiwa na watu wanaolewa dira yake, wanaoweza kuieleza kwa uwazi kanisani na wanaoweza kuusimamia mwili ili ufanye itokee (iwe halisi)."

**Sema**, "Hebu tuangalie kwa kifupi jinsi ambavyo Paulo alikuza na kuimarisha viongozi."

Mmoja asome 2 Timotheo 2:2.

**Sema**, "Kwa Paulo, kukuza Uongozi wa kila Kanisa la mahali pamoja ilikuwa ni muhimu ili kwamba Kanisa liweze kuendelea.

Hivi ndivyo alivyofanya:

- A. Aliwapa Viongozi nafasi. Aliwaweka kuwa wasimamizi wa kazi.
- B. Alijitao kuwaandaa
- C. Aliwaamini

## 3.- MWILI ULIOHAMASISHWA

Tafsiri: Washirika wa Kanisa hufanya kazi pamoja huku wakizitumia karama zao ipasavyo ndani ya kusanyiko na katika jamii.

"Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu. Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una Yeye hata milele na milele. Amina." I Petro 4:10-11

### ***Hatua Tano za Vitendo ili Kuwahamasisha Washirika:***

- I. Andaa uongozi wako ili kulihamasisha kusanyiko zima.
- II. Fundisha juu ya karama za kiroho na uwakili wa vipaji
- III. Bainisha karama na maeneo ya mvuto wa kila mwamini ndani ya kusanyiko.
- IV. Mweke kila mshirika afanye kazi katika huduma au eneo la utumishi
- V. Endelea kuona jinsi maeneo tofauti ya uhai wa Kanisa yanavyoendelea na ufanye marekebisho yanayotakiwa.

UONGOZI - MUNGU -WAPI -WAFUASI - NAFASI - WASIMAMIZI - KUWAANDAA - ALIWAAMINI - MWILI - KARAMA - KUSANYIKO - JAMII - KUSANYIKO - KARAMA ZA KIROHO - VIPAJI - KARAMA - MVUTO - HUDUMA - UTUMISHI - JINSI - MAREKEBISHO

#### **4.- UWAKILI WA RASLIMALI**

Tafsiri: Kanisa linawatia changamoto washirika wake kuwa **mawakili** wazuri wa **mali** zao, **rasilimali** zao na **vitu** vyao. Uwakili ni kutumia vitu hivi na zawadi za kifedha ili kutimiliza kazi ya Ufalme wa Mungu ndani ya **Kanisa** na **jamii** yake.

“Mheshimu BWANA kwa mali zako na kwa malimbuko ya mazao yako yote. Ndipo ghala zako zitakapoja zwa, na mashinikizo yatakapoja zwa na divai mpya.” Mith. 3:9-10.

#### **5.-MUUNGANIKO KATI ANDIKO NA MUKTADHA**

Tafsiri: Kanisa lenye afya linajali muktadha (eneo la kijiografia, kijamii na sababu za kiuchumi, kiutamaduni, nk.). Wakati **ujumbe** wa habari njema za Yesu Kristo haubadiliki, **mbinu** za ushirikishaji zinabadilika.

“Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaadibisha, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema” 2Timotheo 3:16-17

### **KAZI TANO ZA KANISA LENYE AFYA**

#### **1.- UINJILISTI**

Tafsiri: Kanisa **hutangaza** habari njema za Yesu Kristo katika **Neno** na **tendo** na **kuwaalika** watu wawe sehemu ya ufalme wa Mungu. Matendo 1:8.

“Na Bwana akalizidisha Kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa” Matendo 2:47.

#### **2.- UANAFUNZI**

Tafsiri: Kanisa linawasaidia watu kumuona **Mungu** kwa uwazi, kuyajua **mapenzi** yake kwa ajili ya maisha yao na **kuwaandaa** kumfuata Yeye katika nyanja **zote** za maisha. 2Petro 3:18.

“Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume...” Matendo 2:42.

Mambo manne yanayohusiana na Uanafunzi:

1. MWENENDO
2. TABIA
3. MAUDHUI ya Injili
4. KUJITOA

RASLIMALI - MAWAKILI - MALI - RALSIMALI - VITU - KANISA - JAMII - MUKTADHA - UJUMBE - MBINU - UINJILISTI - HUTANGAZA - NENO - TENDO - KUWAALIKA - UANAFUNZI - MUNGU - MAPENZI - KUWAANDAA - ZOTE

### **3.- HUDUMA**

Ufanuzi: Kanisa hushughulika na **mahitaji** ya watu kwa **jina** la Kristo na **kuwaalika** wawe **wanafunzi** wake.

"Wakiuza mali zao na vitu vyao, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja...wakawapendeza watu wote..." Matendo 2:45,47.

#### ***Uhusiano wa aina tatu kati ya Huduma na Uinjilisti.***

- I. Huduma kama **MATOKEO** ya Uinjilisti: Kumfuata Kristo hutufanya tuwe wasikivu kwa mahitaji ya wengine na kujitahidi kuyatimiza.
- II. Huduma kama **DARAJA** kwa Uinjilisti: Huduma kwa wengine kama mwanzo ambaa baadaye huwafanya wawe radhi kuisikia Injili.
- III. Huduma **INAYOAMBATANA** na Uinjilisti: Kunena habari za Yesu huku tukiwahudumia wengine.

### **4.- USHIRIKA**

Tafsiri: Washirika wanasaidia kubebeana **mizigo**, kuonyesha **upendo** na **huruma** ya Kristo.

"Wakawa wakidumu...katika ushirika... Wote walikuwepo pamoja, wakiwa na vitu vyote shirika...Kila siku waliendelea kukutana pamoja kwa moyo mmoja..." Mdo 2:42,44,46

### **5.- IBADA**

Tafsiri: Kanisa hukusanyika kama **familia** ya Mungu ili kukutana na Baba katika **ibada**, **ungamo** na **shukrani**, vile vile kujiweka wakfu kwa **huduma** na **maombi**.

"Wakawa wakidumu...wakiumega mkate na katika kusali...wakimsifu Mungu" Mdo 2:42,47.

HUDUMA - MAHITAJI- JINA - KUWAALIKA - WANAFUNZI - MATOKEO - DARAJA - INAYOAMBATANA - USHIRIKA - MIZIGO - UPENDO - HURUMA - IBADA - FAMILIA - IBADA - UNGAMO - SHUKRANI - HUDUMA - MAOMBI

### ***Shughuli ya Vikundi Vidogo: Ninakumbuka Wakati . . .***

**Muhimu kwa Mwezeshaji:** Kusudi la shughuli hii ni kuwapa washiriki fursa ya kurejea uzoefu wa awali na kuulinganisha na mafunzo mapya.

#### **Maelekezo:**

- Ligawe kundi kubwa kuwa vikundi vidogo nya watu 3 au 4 kwa kila kikundi. Muulize kila mtu katika kikundi kushirikisha uzoefu binafsi kwa habari ya sifa za Kanisa lenye afya ama lisilo na afya. Mwombe kila mmoja kwenye kikundi akamilishe maelezo haya: Ninakumbuka wakati [taja uzoefu] uliotokea; ulinifanya nijisikie [taja hisia], hivyo nika... [taja tendo ulilochukua kwa sababu ya uzoefu], kwa sababu [kwa nini ultenda au ulichukua hatua hiyo].

Mfano wa Uzoefu wa Kanisa Lenye Afya: Ninakumbuka pale Mchungaji wangu alipochukua muda kunilea; ilinifanya nijisikie kuwa wa muhimu kwake na kwa Kanisa, kwa hiyo nikajitolea kufundisha darasa jipya la washirika wapya kwa sababu nilitaka waongofu wetu wapya wajue kwamba wao, vilevile ni wa muhimu katika Kanisa.

Mfano wa Uzoefu wa Kanisa Lisilo na Afya: Ninakumbuka wakati nilipotembelea Kanisa katika mtaa wangu na hakuna hata mmoja aliyenosalimia; ilinifanya nione kama hakuna mtu hata mmoja aliyenijali, kwa hiyo kamwe sikurudi tena kwenye Kanisa hilo kwa sababu ninapenda kuwa katka Kanisa linalojaliana.

*Hapa kuna sentensi yenye kanuni katika mtindo rahisi: Ninakumbuka wakati \_\_\_\_\_; ilinifanya nijisikie \_\_\_\_\_. Hivyo nika \_\_\_\_\_, kwa sababu \_\_\_\_\_.*

- Baada ya kila mmoja kushirikisha uzoefu wake kwenye kikundi, wana kikundi wajadili jinsi gani uzoefu wao unavyohusiana na Tabia ama Sifa 10 za Kanisa lenye Afya ambazo ndio wamejifunza tu.
- Mwisho, funga kipindi kwa kusema, “Katika kozi 12 za mafunzo haya, utajifunza namna ya kuzitumia kila moja ya Sifa 10 katika kazi yako kama mpanda Kanisa ili kwamba mwishoni tusherehekee kwa pamoja kuzaliwa kwa Kanisa jipya lenye afya!”

## KIPINDI CHA 2

### MPANDA KANISA MWENYE AFYA YUKOJE? (DK 60.)

Sema, "Ili kupanda kanisa lenye afya, mpanda Kanisa sharti awe na afya. Katika kipindi hiki tutajifunza juu ya viashiria vitano vya mpanda Kanisa mwenye afya."

### VIASHIRIA VITANO VYA MPANDA KANISA MWENYE AFYA (DK 40.)

Maelekezo:

- Waulize washiriki kujaza mchoro kwenye vitabu vyao unapowashirikisha habari.
- Anza na "Ameitwa na Mungu" na uendelee kuuzunguka mchoro kuelekea kulia.



AMEITWA - IMANI - MWENZI - WENYE MAONO - WAZI - HUJENGA - HUSHIRIKIANA -  
HUJIHUSISHA - HUNYUMBULIKA - WAMEJITO A - MKAMILIFU - KIROHO - KIMFUMO - KIIDADI -  
HUCHOCHEA

## **KUPIMA KIWANGO CHANGU CHA UJASIRI KATIKA UANZISHAJI WA KANISA JIPYA (DK 20.)**

**Muhimu kwa Mwezeshaji:** Kusudi la shughuli hii ni kumsaidia mpanda Kanisa kufikiria juu ya uzoefu wake wa wakati uliopita katika uhusiano na mfano wa mpanda Kanisa mwenye afya.

Waombe washiriki kumalizia maswali yafuatayo ya kujipima na mpango wa kujenga ujasiri (Dk 10.).

(Kulingana na tabia na uzoefu wangu wa wakati uliopita, kama mpanda Kanisa ...)

1.- Nitaitendea kazi imani yangu daima na kudumisha maisha ya ibada yaliyo thabiti.

Low Confidence       Some Confidence       High Confidence

2.- Nitahamasika binafsi na kufanya kazi pasipo uangalizi wa mtu nikiwa kituoni.

Low Confidence       Some Confidence       High Confidence

3.- Ninaungwa mkono na mwenzi wangu.

Low Confidence       Some Confidence       High Confidence

4.- Ninaweza kuiona picha iliyodhahiri ya siku za usoni inayohusiana na upandaji wa Kanisa lenye afya.

Low Confidence       Some Confidence       High Confidence

5.- Ninao uwezo wa kuunda timu inayoweza kuifikia picha ya siku za usoni.

Low Confidence       Some Confidence       High Confidence

6.- Nitajihuisha vema na muktadha wangu wa upandaji Kanisa.

Low Confidence       Some Confidence       High Confidence

7.- Nitajenga mahusiano mazuri ndani ya jamii.

Low Confidence       Some Confidence       High Confidence

8.- Nitanyumbulika katika kushughulika na watu na matukio.

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

9.- Nitaliongoza Kanisa jipya kukua kiroho.

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

10.- Nitaliongoza Kanisa jipya kukua kama shirika lililo bora(kimfumo).

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

11.- Nitaliongoza Kanisa kukua kiidadi kwa njia ya kuifikia jamii kupitia washirika wake.

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

12.- Nitaunda kiwango cha kutosha cha fursa muhimu kwa ajili ya ushirika.

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

13.- Nitaishughulikia migogoro kwa njia yenye afya.

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

14.- Nitawahusisha wengine katika huduma.

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

15.- Nitawasaidia wengine kugundua na kutumia karama zao.

Low Confidence

Some Confidence

High Confidence

## MPANGO WANGU WA KUJENGA UJASIRI

- Ni eneo lipi ambalo ni #1 ninalohitaji kujenga ujasiri sasa?

---

---

---

---

- Ni hatua ipi ninayohitaji kuichukua haraka ambayo itanisaidia kujenga ujasiri katika eneo hili?

---

---

---

---

- Chunguza maeneo yako ulio na Ujasiri Mkubwa. Haya ndio maeneo unayoonekana kuwa na nguvu zaidi kama mpanda Kanisa. Ni hatua zipo unazoweza kuchukua ili kukuza uwezo huu kwa haraka katika jitihada yako ya upandaji wa Kanisa?

---

---

---

---

- Ni nani nimfahamuye ambaye ninaweza kumwomba aniunge mkono kwa maombi na kuniwijibisha ninapofanya kazi ya kujenga ujasiri na kukuza zaidi uwezo wangu?

---

---

---

---

**Maelekezo:**

- Waulize washiriki kujigawa wawili wawili au vikundi nya watatu na kushirikishana yale waliyojifunza juu yao wenyewe kupitia kipindi hiki na kupitia kujipima wenyewe na hatua zipi wanazopanga kuzichukua kuhusiana na waliyojifunza.
- Funga kipindi kwa kuwaomba kuombeana wawili wawili au kimakundi.

**Maelekezo ya Shughuli ya Ziada :**

- Tumia alama za kujipima mwenyewe zilizopo chini ili kuwasaidia washiriki kuzama zaidi katika kuelewa uzoefu wao kuhusiana na Mfano wa Mpanda Kanisa Mwenye Afya.

**Kupima Kiwango cha Ujasiri Wangu kwa Kutumia Alama za Karatasi ya Upandaji wa Kanisa.**

Ujasiri Mdogo	Ujasiri Kiasi	Ujasiri Mkubwa	Alama Zote
Katika kisanduku chini, orodhesha alama za kila swali vile ulivyojibu "Ujasiri Mdogo." Mfano: 1, 6, 7	Katika kisanduku chini, orodhesha alama za kila swali vile ulivyojibu "Ujasiri Kiasi." Mfano: 2, 8, 10.	Katika kisanduku chini, orodhesha alama za kila swali vile ulivyojibu "Ujasiri Mkubwa." Mfano: 3, 11, 15	
Katika kisanduku hapa chini, andika jumla ya idadi ya maswali ambayo ulijibu "Ujasiri Mdogo." Kwa mfano kama ulijibu maswali 3 "Ujasiri Mdogo" andika namba "3" kwenye kisanduku.	Katika kisanduku hapa chini, andika jumla ya idadi ya maswali ambayo ulijibu "Ujasiri Kiasi." Na uzidishe idadi hiyo kwa 2. Kwa mfano, ikiwa ulijibu maswali 3 "Ujasiri Kiasi," zidisha $3 \times 2$ na uandike namba "6" kwenye kisanduku.	Katika kisanduku hapa chini, andika jumla ya idadi ya maswali ambayo ulijibu "Ujasiri Mkubwa." Na uzidishe idadi hiyo kwa 3. Kwa mfano, ikiwa ulijibu maswali 3 "Ujasiri Mkubwa," zidisha $3 \times 3$ na uandike namba "9" kwenye kisanduku"	Kwenye kisanduku hapa chini ,andika jumla ya alama za Ujasiri Mdogo + Ujasiri Kiasi + Ujasiri Mkubwa. Kwa mfano ,ikiwa alama zako zilikuwa Mdogo =3, Kiasi = 6, na Mkubwa = 9, jumla ya alama zako ingekuwa $3+6+9= 18$

**Mpangilio wa Alama:**

Jumla ya Alama za Ujasiri Mdogo: 15-25

Jumla ya Alama za Ujasiri Kiasi: 26-35

Jumla ya Alama za Ujasiri Mkubwa: 36-46

- Pima maswali uliyoyaweka kundi moja katika viwango vitatu vya ujasiri. Je, unauona mpangilio wowote kati ya maswali haya?
- Fikiria jumla ya alama za kiwango chako cha ujasiri. Ni kwa jinsi gani mchanganyiko wa viwango vitatu vya ujasiri unachangia kwenye alama zako za jumla? Je, hali hii inakupa maoni gani kwa habari ya utayari wako wa kupanda Kanisa?

Tafadhali zingatia kwamba hiki ni kifaa cha kujipima, kinachomsaidia mpanda Kanisa kurejea utayari wake kwa ajili ya jukumu la kupanda Kanisa. Kifaa siyo kitabiri mafanikio ama kutokufanikiwa kama mpanda Kanisa. Zaidi, hufungua mlango wa kujipima mwenyewe na mazungumzo yenye matunda kati ya mpanda Kanisa mwenyewe na mwezeshaji wa mpanda Kanisa, mlezi, au msimamizi.

## Kipindi cha 3

### Wazo la “Z” : Mungu Anataka Nini? (Dk.60)

#### WAZO LA “Z” NI NINI? (DK 15 .)

Sema, “WAZO LA ‘Z’ NINI?” “Z”— ni matokeo ya mwisho ya kile ambacho hasa Mungu anakitaka kwa ajili ya taifa, mkoa, jiji, kijiji, au ujirani/mtaa. “Z” inatumika kwa sababu iko mwishoni mwa alfabeti za Kiingereza – herufi ya mwisho ama ya hatima, kama ilivyo Omega inavyomalizia katika herufi za Kiyunani.

#### Maelekezo:

- Waombe washiriki mbalimbali kusoma Isaya 11:9, Isaya 65:12-25 na Ufunuo 21:1-4, 22-27; 22:1-5.
- Waulize jinsi vifungu hivi vinavyoelezea “mwisho wa mchezo” (mwisho mkuu amba Mungu anautaka)?
- Uliza: Ni hatari gani ya kulenga mbingu peke yake na sio katika nchi mpya?
- Waombe washiriki mbalimbali kusoma mistari ya Maandiko yafuatayo kwa sauti: Marko 13:10; Mathayo 24:14; Luka 24:45-47; Wakolosai 1:6; Yohana 3:16; I Timotheo 2:3-4; 2 Petro 3:9 na 2 Wakorintho 5:9.
- Uliza: Mistari hii inatuambia nini juu ya mpango wa Mungu wa kuwafikia watu kwa Injili?
- Uliza maswali haya:
  1. Ni njia zipi ambazo Mungu huzitumia ili kufikia matokeo Yake ya Mwisho anayoyatamani?
  2. Ni chombo gani cha kwanza ambacho Mungu hukitumia ili kufikia matokeo Yake ya mwisho? (Jadili jibu hili pamoja na wengine: “Kanisa Lake.”)
  3. Je, kuna njia nyingine ambayo Mungu anaitumia kwa ubora zaidi leo?
- Waombe washiriki mbalimbali kusoma mistari ya Maandiko yafuatayo kwa sauti: Mathayo 28:18-20, Matendo 1:8, Waefeso 3:10
- Waulize wana kikundi swali lifuatalo: Mistari hii inatuambia nini juu ya kazi yetu ya kutimiliza shauku ya Mungu kwa ajili ya ulimwengu?

## Hatua za Muhimu Katika Kufikia "Z" (Dk .15 )

### Maelekezo:

- Wagawe washiriki katika vikundi vya watu 3 au 4.
- Waombe mtu mmoja mmoja kwa kila kikundi kusoma kwa sauti Maandiko yanayohusiana na kila mojawapo ya mada 5 zifuatazo na mjadili maswali yanayohusiana katika kikundi chao.
- Baada ya dakika 10 za kazi ya vikundi, wape kila kikundi dakika moja ya kushirikisha kwa kifupi pointi za muhimu ambazo wamezijadili.

**A. Maombi |** 2 Nyakati 7:14, Mathayo 9:38

Tuombee nini katika safari yetu ya kuifikia "Z"?

**B. Upendo na Umoja |** Yohana 13:35, Yohana 17:20-23

Kwa nini upendo na umoja ni muhimu ili kuifikia "Z"?

**C. Maono |** Yohana 3:16, 1 Yohana 2:2, Mathayo 9:37

Mistari hii inatuambia nini juu ya maono ya Mungu?

**D. Uinjilisti |** Warumi 10:14-15

Tunawezaji kupata fursa za kuwashuhudia wasioamini katika eneo letu? Je, ni kwa jinsi gani waaminio huvuka mipaka ya marafiki wengine wanaoamini na kuwafikia wasioamini?

**E. Upandaji wa Kanisa |** Waefeso 3:8-11, Waefeso 4:11-13

Je, Mungu anataka watu wake wawe wanafanya nini?

Kanisa jipya linapopandwa, watu hufikiwa katika ujirani au mitaa inayozunguka ambao

wasingeweza kufikiwa pasipo Kanisa jipya. Je, kuna sababu gani za kutokea kwa hili?

Ikiwa unafahamu juu ya hili kutokea, waambie wana kikundi na ujadili kile kilichotokea.

### **Wazo la “Z” Hupelekea Matendo ya “Z” (Dk.15)**

**Sema,** “Matendo mawili yanayotokana na wazo la ‘Z’ ni kupanga na kutoa. ”

**Elezea maswali yafuatayo kwa kifupi.**

1. Ni maswali gani ya kimkakati yanayopaswa kujibiwa ili upandaji wa Kanisa uonekane?
2. Ni mipango gani inayopaswa kufanywa Kanisa linapoelekea katika upandaji wa Kanisa jipya?

### **Kazi ya Vitendo: Mpango Wako wa “Z” (Dk.15)**

#### **Maelekezo:**

- Soma kazi ifuatayo ukiwa pamoja na washiriki.
- Onyesha kwamba matokeo ya kazi hii yatashirikishwa kwenye kikundi katika Funzo la 2.
- Pata muda wa kujibu maswali yote kwa habari ya kazi hii.

#### **Kazi:**

1. Andaa au tafuta ramani ya jiji lako au kijiji unachopanga kupanda Kanisa.

Onyesha makanisa ya kiinjili mengi uwezavyo katika jiji au kijiji na uonyeshe ukubwa wake kwa makisio juu ya ramani. Chunguza idadi ya watu wa jiji au kijiji.

Viongozi wa Kikristo wamesema kwamba ili nchi iwe na “mpenyo,” wa Kanisa inapaswa kuwa na Kanisa moja la kiinjili kwa kila watu 1,000. Ikiwa tutakubaliana na wazo kwamba tunapaswa kuwa na Kanisa moja kwa kila watu 1,000, unafikiri ni makanisa mangapi zaidi yatahitaji kupandwa kwenye jiji au kijiji unachopanga kupanda Kanisa?

2. Anza kufikiria juu ya mpango wa Kanisa lako kwa ajili ya jitihada ya upandaji wa Kanisa inayojumuisha maombi, umoja na upendo, maono, uinjilisti, na upandaji wa Kanisa. Andika mawazo ya awali na umshirikishe mlezi wako au mkufunzi wa kipindi hiki.

3. Fikiria juu ya mtaa, kijiji, jiji, mkoala, au nchi. Fikiri majibu ya maswali:

- “Mungu anataka nini kwa ajili ya \_\_\_\_\_ (taja jina la jiji, kijiji, au mtaa unaopanga kupanda Kanisa)? Andika jibu katika kifungu kimoja.
- Orodhesha mambo matatu utakayoyafanya ili kusaidia uione “Z” ikitokea katika eneo lako.

### **Kuifikia “Z Kutoa”!**

#### **Maelekezo:**

- Waombe washiriki kusoma 2 Wakorintho 8:7; 2 Wakorintho 9:6-7.
- Jadili swali lifuatalo.

Tunawezaji kuwa na uhakika kwamba fedha zinazohitajika kwa ajili ya upandaji wa Kanisa zitatolewa?

- Shirikisha kanuni zifuatazo zinazohusiana na kuchangia kanisa linalopandwa na njia za kutafuta fedha kwa ajili ya upandaji wa Kanisa.
- Waombe washiriki kujaza nafasi zilizo wazi katika vitabu vyao.

**Sema**, “Kuna dhana mbili muhimu kwa habari uchangiaji wa Kanisa linalopandwa.”

Kanuni Mbili Katika Kulichangia ama Kulifadhili Kanisa Linalopandwa

#### **1. Mwamini Mungu**

#### **2. Utoshelevu**

- Waombe washiriki kusoma Wafilipi 4:6-7; 11-13, 19 na kujadili kwa kifupi uhusiano wao na kanuni hizi.
- Kisha washirikishe darasa njia zifuatazo za kulifadhili Kanisa linalopandwa.

Njia za kulifadhili Kanisa Jipya:

1. Ufadhilli kutoka Kanisa **mama**.
2. Ufadhilli kutoka kwenye **dhehebu**, **misheni** au **shirika**.
3. Kikundi **maalumu** cha ufadhilli.
4. Ufadhilli wa kutoka kwa **wawekezaji**, **marafiki** na **ndugu**.
5. Ufadhilli kutoka katika **bidhaa** zilizouzwa.
6. Ufadhilli kutoka mshahara wa **pili** katika kaya/nyumba.
7. Kufanya huduma huku ukifanya **kazi nyiningine**.


Chakula cha Mchana (Dk. 60)

## KIPINDI CHA 4

### MZUNGUKO WA UPANDAJI WA KANISA (DK.60)

**Maelekezo kwa Mwezeshaji:** Kwa kutumia mchoro wa Mzunguko wa Upandaji Kanisa uliopo chini, toa muhtasari wa mzunguko wa upandaji wa Kanisa.

#### Mzunguko wa Upandaji Kanisa



Shughuli ya Vikundi vidogo (Dk. 25 )

**Maelekezo:**

- Gawa katika makundi 7 ( Kundi 1 kwa kila awamu). Wape awamu moja kila kundi.
- Waombe kila kundi kusoma kwa sauti vifungu vyta Biblia vinavyohusiana na awamu yao.
- Waaelekeze kundi kuandaa vitendo vingi iwezekanavyo ili watoe “Shughuli” na “Masuala ya Msingi” yanayohusiana na kila awamu.

**AWAMU YA I: Maombi** (Luka 10:2, Waefeso 6:18-19, Wakolosai 4:2-4)

**SHUGHULI:**

- Anza na maombi.
- Waonyeshe mtu ambaye watafanya uinjilisti na upandaji Kanisa pamoja.

- Omba kwa ajili ya wale watakaosaidia na kwa ajili yako mwenyewe.

#### MASUALA YA MSINGI

- Shamba langu binafsi la mavuno ni lipi? Je, Mungu anataka nini kutoka kwangu katika eneo langu?
- Ni mambo gani yanayohusiana na wito na maono ambayo Mungu ananipa yaliyo tofauti na yale anayowapa watu wengine?
- Ni nani atasaidia?
- Niombe kwa ajili ya nani? Niombe kwa ajili ya nini?
- Nimwombe Mungu afanye nini katika huduma yangu kwa ajili yake ?

#### **AWAMU YA II: Fanya Uinjilisti** (1 Wakorintho 9:19-23; Matendo 1:8)

##### SHUGHULI:

- Kutana na viongozi muhimu na ujenge mahusiano.
- Fanya Uinjilisti kwa waliopotea.
- Anzisha masomo ya Biblia ya kikundi cha kiinjilisti.
- Waonyeshe waumini wapya jinsi ya kufanya huduma kwa njia unayofanya wewe.

##### MASUALA YA MSINGI:

- Ni mbinu zipi za kiinjilisti zinafaazaidi kwa ajili yetu kufikia malengo yetu?
- Tunakutanaje na viongozi muhimu? Ni akina nani?
- Tunawapataje?
- Tunawafunzaje waumini wapya kuwa mashahidi kwa marafiki na familia zao?
- Tunawajuje marafiki wa waumini wapya na kuanza kuwainjilisha /kuwahubiri?

#### **AWAMU YA III: Fanya Wanafunzi** (1 Wathesalonike 5:11; Mathayo 28:18-20)

##### SHUGHULI :

- Fundisha waumini wapya.
- Lea viongozi wanaobukia.
- Fundisha utii na kujitolea kwa Bwana.
- Watie moyo waumini kumfanania Kristo.
- Wafundishe waumini wapya kumtii Kristo.

##### MASUALA YA MSINGI:

- Ni jinsi gani ya kukuza na kuwafundisha kikundi cha watu?

- Ni jinsi gani ya kuwa kielelezo cha uongozi ulio bora?

#### **AWAMU YA IV: Kukusanyika Pamoja (Waebrania 10:24-25)**

SHUGHULI:

- Panua jitihada za uinjilisti kupitia mtandao wa marafiki.
- Zidisha vikundi kiini kwa kuhakikisha kila kikundi kiini kinaanzisha vikundi vingine.
- Anzisha mfumo wa ibada endelevu.

MASUALA YA MSINGI:

- Ni jinsi gani viongozi wa kikundi kiini kipyा watafunzwa na kuachiliwa?
- Ni lini tunawabatiza waumini wapya? Ni wakati gani na ni nani anayewapa ushirika?
- Tutaanzishaje ushirika wa karibu wa waamnio? Waumini wapya wataletwaje katika ushirika?
- Wakati tunapokusanyika, tunakutanikia wapi? Tunawakaribishaje watu?
- Ni utaratibu gani ambao tutautumia ili kufikia kusudi letu lengwa?
- Ni mtindo gani wa ibada ambao tutautumia?

#### **AWAMU YA V: Kuza Viongozi (2 Timotheo 2:2)**

SHUGHULI:

- Andaa muhtasari wa viongozi wanaohitajika kwa kila eneo la huduma.
- Chunguza na uandike karama za kiroho za washirika wote.
- Wafunze viongozi wa vikundi kiini.
- Wape kazi na uwaachilie viongozi kwenye huduma.
- Andaa muundo na nafasi za kihuduma unazolenga kwa ajili ya huduma.
- Fanya ufuatiliaji pamoja na viongozi ili kutoa msaada.

MASUALA YA MSINGI

- Tunawahusishaje waumini wapya kugundua karama zao za kiroho? Ni nani atakayewafunza?
- Ni maeneo gani ya mafunzo ambayo yanahitajika? Ni wapi na ni kwa namna gani mafunzo haya yatatolewa?
- Viongozi muhimu wenyе uwezo ni akina nani? Karama zao na uwezo wao ni upi? Je, ni waaminifu, wanawatumikia watu?
- Je, wale waliofunzwa watafanya huduma wapi? Mahitaji ya msingi na masuala

mengine katika eneo hilo ni yapi? Huduma yao katika eneo hilo itaanza lini?  
 Watatoa taarifa kwa nani? Kazi zao au majukumu yao ni yapi?

### **AWAMU YA VI: Zidisha (Matendo 1:8)**

#### SHUGHULI:

- Wafunze viongozi namna ya kuunda timu ya upandaji wa Kanisa.
- Wafunze watenda kazi kwa ajili ya aina mbalimbali za huduma zinazoambatana na upandaji wa Kanisa.
- Fanya utafiti wa mikoa ambayo watu wanaongozwa kuanzisha huduma.
- Panga na uendeshe jitihada za uinjilisti katika mikoa mipya.
- Anzisha na kuchagua viongozi watakaofanya kazi pamoja nasi kwa ajili ya huduma.

#### MASUALA YA MSINGI:

- Ni utafiti gani unaohitaji kufanyika? Ni nani atakayeufanya? Je, kuna makundi au makabila yaliyo jirani ambayo hayajafikiwa na injili? Je, kuna viongozi wenye uwezo wanaoweza kufunzwa?
- Ni malengo gani yanahitaji kuwekwa na kutolewa kwa watu sahihi? Ni nani anayeongoza jitihada ya maombi ili kuunga mkono huduma hii?
- Ni nani anayetua majukumu na kusimamia huduma za upandaji wa Kanisa jipya?
- Je, tunahitaji huduma zozote za mafunzo ya nyongeza ili kutoa mafunzo ya uongozi katika viwango tofauti kwa ajili ya harakati hii? Ni nani atakayetua mafunzo? Je, yatafadhiwaje?

### **AWAMU YA VII: Harakati (Isaya 11:9)**

#### SHUGHULI:

- Yafikie makabila yote ya nchi.
- Weka miongozo ili kukuza harakati.
- Amua juu ya miradi ya umisheni wa nje ambayo kikundi kitaifadhili.
- Endesha makongamano ya maombi na kusifu.
- Weka malengo ya kimkoaa na/au kitaifa.
- Anzisha viwango vya juu vya mafunzo kwa ajili ya viongozi muhimu wa harakati.

**MASULA YA MSINGI:**

- Je, harakati inajiendeleza yenyewe, inajitegemea kifedha, na inajiongoza yenyewe? Kama sivyo, nini kifanyike ili kuhakikisha inafanya mambo haya?
- Je, ni mikoa ipi au watu ambao hawajafikiwa? Je, ni miradi gani ya kimisheni ambayo Bwana anatuongoza kuianzisha?
- Ni aina gani ya mafunzo yanayohitajika kwa ajili ya harakati? Je, yatafadhliliwaje?
- Je, ni nani walio viongozi wa “aina ya kitume” kwa ajili ya harakati? Tunawezaje kutenda kazi pamoja nao? Je, tunawezaje kuwatia moyo na kuwaunga mkono? Mahitaji yao ni yapi?

**Utoaji wa ripoti ya Kundi kubwa (Dk.30 )**

Maelekezo:

- Wape dakika 5 kila kikundi kidogo kutoa mawazo yao kwenye kundi kubwa kwa ajili ya hatua ama vitendo vinavyohusiana na kazi zao za awamu .

## KIPINDI CHA 5

# KWA NINI VIKUNDI VIDOGO? (DK. 60)

### Misingi ya Kibiblia juu ya Vikundi Kiini

Sema, "Matumizi ya vikundi vidogo vya kujifunza Biblia kwa ajili ya uinjilisti na uanafunzi ndicho kiini katika mbinu za upandaji wa Kanisa lenye afya zitakazofundishwa katika kozi hii. Katika kozi nyingine za upandaji wa Kanisa, tofauti hutolewa kati ya maneno 'kikundi kiini' na 'kikundi kidogo.' Katika kozi hii, tutatumia neno 'kikundi kidogo' lakini tukilififikiria kuwa kitu kimoja na 'kikundi kiini.'

Tunakielezea kikundi kidogo (au kikundi kiini) kuwa ni kikundi kidogo cha watu amba hukusanyika pamoja ili kujifunza Neno la Mungu kwa makusudi ya uinjilisti, uanafunzi, na huduma, kuchangia uundwaji wa Kanisa lenye afya, linaloabudu.

Maelekezo:

- Waulize kundi kubwa maswali yafuatayo:
  1. Je, kulikuwa na vikundi kama vile tunavyoviita vikundi vidogo katika Agano Jipya?
  2. Ni mambo gani yanayokifanya kikundi kidogo cha Kikristo kuwa tofauti na vikundi vingine?

Shughuli ya Ugunduzi ya Vikundi Vidogo vya Biblia (Dk.15)

Maelekezo:

- Jigaweni katika vikundi 4.
- Wape kila kikundi swali na maandiko ya Biblia yaliyooneshwaa.
- Waombe kila kikundi kusoma vifungu vya Biblia, kujibu swali lao, na kuiandaa kutoa taarifa ya jibu lao kwa kifupi kwenye kundi kubwa.
- Waombe vikundi vyote wafanye kazi kwenye chumba kimoja.
- Zingatia kuwa kila kikundi kitakuwa na dakika kumi kukamilisha shughuli hii.
- Baada ya dakika 10 (pasipo kuunda tena kundi kubwa), waulize kila kikundi kidogo kutoa taarifa kwa kifupi ya namna walivyojibu maswali yao.

**Kikundi A:** Je, ni zipi baadhi ya kazi za kiinjilisti za vikundi vidogo vya Agano Jipya?  
(Matendo 4:20; 5:42; 20:20)

**Kikundi B:** Je, baadhi ya kazi za uanafunzi za Agano Jipyä ni zipi? (Matendo 6:4, Wakolosai 4:17)

**Kikundi C:** Baadhi ya kazi za ushirika za vikundi vidogo vyä Agano Jipyä ni zipi? (Matendo 2:42, Waebrania 10:25, Matendo 20:7, 11)

**Kikundi D:** Baadhi ya kazi za ibada za vikundi vidogo katika Agano Jipyä ni zipi? (Matendo 1:14; 2:47; 6:4; Wakolosai 4:2)

### **Faida za Vikundi Vidogo (Dk.40 )**

#### **Mjadala wa Kikundi Kidogo(Dk. 20)**

Maelekezo:

- Wakiwa katika vikundi vile vile vidogo kama ilivyo hapo juu, wape maswali yafuatayo kila kikundi.
- Waombe kila kikundi wajipange kuwashirikisha vikundi vingine majibu yao.
- Waombe kila kikundi waandike majibu yao kwenye karatasi kubwa, kama zinapatikana, zinazoweza kubandikwa kwenye kuta za chumba.

**Kikundi A:** Faida za vikundi vidogo kwa ajili ya uinjilisti ni zipi?

Baadhi ya shughuli za vikundi vidogo zitakazowawezesha kuwafikia watu kwa habari njema za Kristo ni zipi?

**Kikundi B:** Faida za vikundi vidogo kwa ajili ya uanafunzi ni zipi?

Baadhi ya shughuli za vikundi vidogo zinazowezekana ambazo zitaleta matokeo ya masaidiano, mafundisho na malezi ni zipi?

**Kikundi C:** Faida za vikundi vidogo kwa ajili ya ushirika ni zipi?

Baadhi ya shughuli za vikundi vidogo zinazowezekana ambazo zitazalisha hali ya kutiana moyo, kushirikishana, na urafiki katika Kristo ni zipi?

**Kikundi D:** Faida za vikundi vidogo kwa ajili ya ibada ni zipi?

Baadhi ya shughuli za vikundi vidogo zinazowezekana ambazo zitamtukuza na kumwadhimisha Mungu ni zipi?

### Taarifa na Mjadala wa Kundi Kubwa (Dk.20 )

Maelekezo:

- Baada ya dakika 20 (washiriki waendelee kukaa katika vikundi vidogo), waulize kila kikundi kidogo kutoa taarifa kwa ufupi juu ya jinsi walivyojibu maswali yao (dk.10).
- Katika kufunga kipindi, waongoze vikundi katika mjadala wenye maswali yafuatayo:
  1. Faida za vikundi vidogo katika kukuza viongozi ni zipi?
  2. Kwa kusimamia yote tuliyojifunza katika kipindi hiki, unawezaje kutoa muhtasari wa faida za vikundi vidogo kwa ajili ya upandaji wa Kanisa?

### Pumziko (Dk.15 )

# KIPINDI CHA 6

## KUACHA BIBLIA ITUFUNDISHE (DK.60)

### Mbinu ya Kujifunza Biblia kwa Njia ya Uchimbuzi, Sehemu ya 1 (Dk. 60.)

Uchimbuzi dhidi ya Uchambuzi (2 Tim. 2:15) (10 min.)

Maelekezo ya Muhtasari ya Mwezeshaji: Kwa kutumia dondoo hapa chini, elezea tofauti kati ya mtindo wa uchimbuzi na uchambuzi katika kujifunza Biblia.

#### 1. Mtindo wa Uchambuzi

I. Kufikiri Kiuchambuzi.

Tunaanza na wazo linalojulikana na linalokubalika na tunatoa kutoka humo (“tunachomoa”) hitimisho.

II. Kujifunza Biblia kwa njia ya Uchambuzi

Mwalimu huelezea sheria ya jumla kwamba katika Agano Jipy, hamira (au chachu) mara nyingi humaanisha dhambi. Tunaposoma Mathayo 13:33, tunadhani kwamba hamira inazungumzia dhambi. Soma kifungu. Je, hamira hapa inamaanisha dhambi?

III. Mbinu ya Mfano

Waalimu wa Biblia mara nyingi wanajua wanachotaka kukisema, na huja tu kwenye Biblia ili kupata mstari wa kuunga mkono mawazo ama uelewa wao. Kwa nini hili linaweza kuleta hatari ya kutokuelewa maana halisi ya kifungu?

#### 2. Mtindo wa kuchimbua

I. Kufikiri kiuchimbuzi

Tunapima kweli kwa ukaribu ili kujaribu kuelewa kweli maana yake.

II. Kujifunza Biblia kwa njia ya Uchimbuzi

Tunapima kwa uangalifu andiko na muktadha wa Mathayo 13:33 ili kuamua ni nini ambacho neno “hamira” au “chachu”linamaanisha.

III. Uchimbuzi ndio Mbinu Iliyo Bora

Tunapowasaidia watu kugundua kweli za Biblia wanapojifunza, mbinu ya uchimbuzi ndilo chaguo lililo jema.

## Hatua za Kujifunza Biblia kwa Kuchimbua (Dk.20)

Maelekezo:

- Waulize washiriki kukamilisha dondo zifuatazo kwenye vitabu vyao wakati unapowashirikisha maneno yasiyokuwepo.

A. Uchunguzi – Je, *inasemaje?*

B. Tafsiri – Je, *ina maana gani?*

C. Matumizi – Je, *ninapaswa kufanya nini?*

## Dondoo za Kujifunza Biblia kwa Uchimbuzi

**Jenga Msingi ulio Imara.**- Hii huanza na uchunguzi mpana. Pima kwa uangalifu maudhui ya kifungu ili kuamua maana yake halisi ili kwamba mtu aweze kufanya matumizi ya andiko yaliyo sahihi.

**Pata muda wa kutosha wa kujifunza.**- Usianze na usomaji wa haraka haraka na ukahisi kwamba unajua maana yake ni nini. Usifanye matumizi ya haraka na yenye maswali ya kile ambacho andiko linafundisha.

**Maelekezo ya Mwezeshaji:** Kwa hatua hii, waulize washiriki ikiwa wana maswali juu ya mbinu za kujifunza Biblia kwa njia ya uchunguzi. Pata muda wa kujibu maswali yao ipasavyo.

## Mfano wa Kujifunza Biblia kwa Uchambuzi (Dk.25)

Muhtasari wa Maelekezo ya Mwezeshaji: Liongoze darasa kwenye Funzo la Biblia kwa njia ya Uchimbuzi kutoka Yohana 1: 1-5 kwa kifupi. Hakikisha unatia moyo mchakato wa ushiriki. Waombe washiriki kuandika mambo muhimu juu ya kifungu kwenye dondo zilizotolewa kwenye vitabu vyao.

**John 1:1-5**  
Kujifunza Biblia Kwa Njia ya Uchimbuzi

A.- Uchunguzi: Je, kifungu kinasemaje?

---

---

---

---

B.- Tafsiri: Je, kifungu kina maana gani?

---

---

---

---

C.- Matumizi: Je, ninapaswa/ tunapaswa kufanya nini?

---

---

---

---

**Kazi ya Nyumbani:** Kujifunza Biblia Kibinafsi Kwa Njia ya Uchimbuzi (Dk.5.)

Katika maandalizi ya somo la kujifunza Biblia kwa njia ya uchimbuzi linalofuata juu ya uchunguzi, chukua kifungu kifupi cha Andiko ili kujifunza (si zaidi ya paragrafu). Tumia angalau saa 1 kuchunguza kifungu ukiwa katika hali ya maombi na kumwomba Mungu akufungue macho yako kwa mambo ambayo bado hujayaona. Nakili uchunguzi wako. Je, ulijifunza nini? Jiandae kushirikisha uzoefu wako kwa wenzako kwenye kipindi kinachofuata cha mafunzo.

## KUFUNGA

- Pitia kazi mbili za vitendo kazini (angalia kipindi cha 3 na cha 6). Jibu maswali yote yanayohusiana na kazi hizo.
- Omba watu wa kujitolea ili washirikishe majibu ya maswali yafuatayo kwa maneno yao wenyewe:
  1. Kanisa lenye afya ni nini? (angalia Kipindi cha 1)
  2. Hatua za msingi za kupanda Kanisa lenye afya ni zipi? (angalia kipindi cha 4)
  3. Kwa nini kupanda Kanisa lenye afya ni muhimu? (mchoro juu ya vipindi vyote)
- Waombe washiriki kuchangia kitu walichojifunza katika mafunzo ambacho kiliwasismua, kiliwatia moyo ama kiliwapa motisha kwa ajili ya kazi yao kama wapanda Kanisa.
- Imbeni wimbo wa kuabudu kwa pamoja na mfunge kwa maombi ya baraka kwa ajili ya wapanda Kanisa hawa.

### Ni nini kinachofuata?

Kabla hujafika kwenye kipindi cha mafunzo kinachofuata, tunapendekeza ufanye yafuatayo:

- Kutana/Fikia watu 10 wapya.
- Peleka injili kwa watu 5.
- Anzisha kikundi kidogo kipyta.

Mpango Kazi kwa ajili ya Funzo #2: Mambo Muhimu:

- Kamilisha Mpango Kazi wa “Z” (angalia Kipindi cha3).
- Pata muda wa kujifunza Biblia kwa njia ya uchimbuzi (angalia Kipindi cha 6).